



Zama anajitayarisha
kwenda shule.



Baba anapika uji wa
kiamsha kinywa.



"Mama hutayarisha
uji mzuri zaidi."
Zama anasema.

Uji unampa Zama nguvu
za kucheza shulenii.





Uji uko tayari.



Baba anaongeza uji
maziwa kwa
upendo.



"Baba, ninafikiri uji
huu unahitaji sukari
zaidi," Zama
anasema.



"Uji wa mama una
ladha kuliko wa
baba," Zama
anawaza



"Baba, tafadhali
naweza kupata
sukari zaidi?" Zama
anauliza.



Baba
anamwongeza
Zama 'sukari.'



“Wu! Baba!
Umeweka chumvi
badala ya sukari!”
Zama analalamika.



“Baba, je, mama
atarudi lini
nyumbani?” Zama
anauliza.